TANGAZO LA SERIKALI NA. 229 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA YA 283)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 121(a) na (f))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UWINDAJI WA KITALII ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 780 la 2024

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za Mwaka 2024 ambazo katika Kanuni hizi zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya jumla

2. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa ujumla kwa kufuta neno "mnyama" popote linapotokea na badala yake kuweka neno "mnyamapori".

Marekebisho ya kanuni ya 2

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 2 kwa kuongeza maneno "Tanzania, chini ya Sheria ya Kampuni" mara baada ya neno "iliyosajiliwa" lililopo katika tafsiri ya msamiati "kampuni ya uwindaji".

Marekebisho ya kanuni ya 3

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3(1) kwa kufuta maneno "na atatoa cheti kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza".

Marekebisho ya kanuni ya 5

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5(1) kwa kufuta rejea "kanuni ndogo ya (3)" na badala yake kuweka rejea "kanuni ya 3".

Marekebisho ya kanuni ya 8

6. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 8-
(a) katika kanuni ndogo ya (1), kwa kuongeza

maneno "katika tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii za Wizara na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori" mara baada ya neno "vilivyowazi";

(b) katika kanuni ndogo ya (4), kwa kuongeza neno "isiyorejeshwa" mara baada ya neno "kitalu"; na

(c) katika kanuni ndogo ya (9), kwa-
   (i) kufuta aya (b); na
   (ii) kupanga upya aya (c) na (d) kuwa aya (b) na (c).

Marekebisho ya kanuni ya 9

7. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 9(1) kwa kufuta neno "Mkurugenzi" na badala yake kuweka neno "Waziri".

Marekebisho ya kanuni ya 10

8. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 10-

(a) katika kanuni ndogo ya (3)(g), kwa-
   (i) kufuta maneno "samani zingine za lazima" yaliyopo katika aya ndogo ya (vi) na badala yake kuweka maneno "samani nyingine muhimu ikiwemo vitanda, meza na viti"; na
   (ii) kufuta rejea "aya ya (h)" yaliyopo katika kivuo na badala yake kuweka rejea "aya (g)";

(b) katika kanuni ndogo ya (3)(h), kwa-
   (i) kufuta maneno "samani zingine za muhimu" yaliyopo katika aya ndogo ya (vii) na badala yake kuweka maneno "samani nyingine muhimu ikiwemo vitanda, meza na viti"; na
   (ii) kufuta maneno "hapo juu" yaliyopo katika kivuo na badala yake kuweka maneno "vilivyoainishwa katika aya hii";

(c) kwa kupanga upya kanuni ndogo ya (3) iliyojirudia kuwa kanuni ndogo ya (4); na

(d) katika kanuni ndogo ya (4) iliyopangwa upya, kwa kufuta rejea "kanuni ndogo ya (1)" na badala yake kuweka rejea "kanuni ndogo ya (2)".

Marekebisho ya kanuni ya 14

9. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 14 kwa-

(a) kufuta neno "maombi" katika kanuni ndogo ya (6) na badala yake kuweka maneno "kibali cha utalii wa uwindaji"; na
(b) kufuta kanuni ndogo ya (8).

Marekebisho ya kanuni ya 16

10. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 16(8) kwa-

(a) kuongeza maneno "na kuiwasilisha kwa Mkurugenzi" mara baada ya neno "Saba" lililopo mwishoni mwa aya (a);
(b) kufuta aya (b) na badala yake kuweka aya mpya ifuatayo:
  "(b) endapo safari itahusisha uwindaji wa simba, kujaza fomu ya kurudi safari ya kuwinda simba iliyoainishwa katika Jedwali la Nane na kuiwasilisha kwa Mkurugenzi."; na
(c) kufuta aya (c).

Marekebisho ya kanuni ya 19

11. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 19 kwa-

(a) kuongeza maneno "aliyeuawa au kujeruhiwa" mara baada ya neno "mnyamapori" lililopo kwenye maelezo ya pembeni;
(b) kuongeza maneno "aliyeuawa au kujeruhiwa" mara baada ya neno "mnyamapori" lililopo katika kanuni ndogo ya (1);
(c) kuongeza maneno "aliyeuawa au kujeruhiwa" mara baada ya neno "mnyama" lililopo katika kanuni ndogo ya (2); na
(d) kuongeza maneno "waliouawa au kujeruhiwa" mara baada ya neno "wanyamapori" lililopo

katika kanuni ndogo ya (3).

Marekebisho ya kanuni ya 20

12. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 20 kwa kufuta neno "maalum" popote linapojitokeza katika kanuni hiyo na badala yake kuweka neno "muhimu".

Marekebisho ya kanuni ya 23

13. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 23 kwa-

(a) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (7) kanuni ndogo mpya ifuatayo:

"(8) Endapo Waziri hataridhia ombi la uhamishaji wa kitalu atamjulisha muombaji kwa maandishi."; na

(b) kupanga upya kanuni ndogo ya (7) iliyojirudia na kanuni ndogo ya (8) kuwa kanuni ndogo za (8) na (9) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 24

14. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 24(1) kwa kuongeza maneno "ya muda" mara baada ya maneno "uwindaji kabla".

Marekebisho ya kanuni ya 29

15. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 29(4)(b) kwa-

(a) kufuta neno "tano" lililopo katika aya ya (ii) na badala yake kuweka neno "saba"; na

(b) kufuta neno "tano" lililopo katika aya ya (iii) na badala yake kuweka neno "kumi".

Marekebisho ya kanuni ya 31

16. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 31 kwa kuongeza maneno "kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Nne" mara baada ya maneno "kuanzia siku ya uamuzi" yaliyopo mwishoni mwa kanuni ndogo ya (1).

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

17. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Kwanza na kuliandika upya kama ifuatavyo:

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 8(8)(b) na 9(9)(b))*

CHETI CHA UGAWAJI WA KITALU CHA UWINDAJI

Sehemu kilipotolewa: ……………………..…………………………………………………………..

Tarehe ya kutolewa: ………………………………………..…………………………………….

Tarehe ya kumaliza muda wa matumizi (inategemea uzingatiaji wa kanuni): …..……………………..

Imetolewa kwa: ……………………..……………………………………………………………….

Jina la kampuni na anuani: ……………………..……………………………………..…………

Maelezo ya mipaka ya kitalu cha uwindaji: …………………………………………………...………………………….……………………………
……………………...………………………..……………………………………………………………

Masharti maalum yanayoambatana na kitalu au vitalu vya uwindaji:

(a) Kufuata masharti ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283;
(b) Kutii masharti ya Kanuni za Uwindaji wa Watalii za mwaka 2024 kuhusiana na uendeshaji wa shughuli za uwindaji;
(c) Kulipa ada ya mwaka ya kitalu cha uwindaji sawa na dau lililofikiwa katika mnada wa kitalu hicho;
(d) Kulipa kwa wakati ada na michango mingine yote inayohusiana na shughuli za uwindaji wa kitalii kama inavyoelekezwa chini ya sheria;
(e) Kuchangia uboreshaji wa miundombinu na ulinzi wa mazingira ndani ya kitalu;
(f) Kuchangia oparesheni za kuzuia ujangili au kupambana na shughuli nyingine yeyote haramu inayohusu uhifadhi wa wanyamapori; na
(g) Waziri anaweza kufuta ugawaji wa kitalu cha uwindaji ikiwa kutatokea tukio lolote lililoainishwa chini ya kifungu cha 38(12)

cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 au Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za Mwaka 2024.

……………………..……………
Saini ya Waziri na Mhuri wa ofisi

Kufuta na kuliandika upya Jedwali la Tano

18. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Tano na kuliandika upya kama ifuatavyo:

__________

JEDWALI LA TANO

__________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 14(2))*

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UTALII WA UWINDAJI

| Taarifa za Kampuni | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Jina la Kampuni | | | | | |
| Anuani | | | | Barua pepe: | |
| Jina la Mtu wa Kuwasliiana naye | | *Namba ya Simu* | | Barua pepe: | |
| | | | | | |

| Maelezo ya Mteja | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jina la Mteja (Kamili) | | | | Jinsia | | Umri | |
| Na. ya pasi ya kusafiria | | *Sehemu ilipotolewa* | | | *Uraia* | | |
| Kazi | | *Anuani ya barua pepe* | | | | | |

**Maelezo ya Safari ya Uwindaji**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Majina ya Mwindaji Bingwa (PH) | | Daraja la leseni ya PH ☐ | Namba ya leseni ya PH ☐☐☐ ☐☐ |
| | | | |

| | | |
|---|---|---|
| Jina la kitalu/vitalu vya uwindaji ambapo uwindaji utafanyika | 1 | |
| | 2 | |
| | 3 | |
| | 4 | |
| | 5 | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kifurushi cha Safari (chagua moja) | *Regular* (Siku 10) | *Major* (siku 14) | *Premium* (siku 21) | Uwindaji ndege | Siku za ziada | Tarehe | Kuanzia | |
| | | | | | | | Hadi | |
| | | | | | | | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Maelezo ya silaha | | Aina | *Calibre* | *Make* | *Maker's No* | Na. ya kibali cha kuingiza nchini | Sehemu kilipotolewa | Tarehe ilipotolewa |
| | 1 | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | |
| | 3 | | | | | | | |
| | 4 | | | | | | | |

**Orodha ya Watazamaji (Awe na miaka 6 na kuendelea)**

| Na | Jina | Umri | Uraia | Na. ya pasi ya kusafiria | Na. siku | Kuanzia tarehe | Hadi tarehe |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | |
| 3 | | | | | | | |
| 4 | | | | | | | |
| 5 | | | | | | | |
| 6 | | | | | | | |
| 7 | | | | | | | |

Ninathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni sahihi kwa uelewa wangu na ninathibitisha kwamba ninaelewa matakwa ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 na kanuni zake.

Tarehe: ………………………….

…………

……………………………

Jina na Sahihi ya Mwombaji na Muhuri wa Ofisi

ORODHA YA WANYAMAPORI

| Na. | Kiingereza | *Jina la Kisayansi* | Kiasi | Eneo atakapowindwa (ikiwa tofauti na kibali mama) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baboon Yellow | *Papio Anubis* | | |
| 2 | Baboon Olive | *Papio cynocephalus* | | |
| 3 | Buffalo African cape | *Syncerus caffer caffer* | | |
| 4 | Bushbuck Chobe | *Tragelaphus scriptus omatus* | | |
| 5 | Bushbuck Masai | *Tragelaphus scriptus* | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | *delameri* | | |
| 6 | Bushpig | *Potamochoerus larvatus* | | |
| 7 | Caracal | *Caracal caracal* | | |
| 8 | Civet African | *Civettictis civetta* | | |
| 9 | Crocodile Nile | *Crocodilus niloticus* | | |
| 10 | Dikdik Kirk's | *Madoqua kirkii kirkii* | | |
| 11 | Duiker Abbott's | *Cephalophas spadix* | | |
| 12 | Duiker Common | *Sylvicapra grimmia abyssinicus* | | |
| 13 | Duiker Harvey's red | *Cephalophas natalensis* | | |
| 14 | Eland Livingstones | *Tragelaphus oryx livingstoni* | | |
| 15 | Eland Paterson's | *Tragelaphus oryx pattersonius* | | |
| 16 | Elephant African | *Loxodonta Africana* | | |
| 17 | Fox Bat eared | *Otocyon megalotis* | | |
| 18 | Gazelle Grant's | *Nanger granti granti* | | |
| 19 | Gazelle Robert's | *Nanger granti robertsi* | | |
| 20 | Gazelle Thomson's | *Eudorcas thomsonii* | | |
| 21 | Genet Blotched | *Genetta tigrina* | | |
| 22 | Genet Common | *Genetta genetta* | | |
| 23 | Gerenuk | *Litocranius walleri walleri* | | |
| 24 | Grysbock Sharpe's | *Raphicerus sharpie* | | |
| 25 | Hare Scrub | *Lepus capensis* | | |
| 26 | Hare Cape | *Lepus saxatilis* | | |
| 27 | Hartebeest Coke's | *Alcelaphus buselaphus cokii* | | |
| 28 | Hartebeest Lichteinstein's | *Alcelaphus buselaphus lichtensteinii* | | |
| 29 | Hippo | *Hippopotamus amphibius* | | |
| 30 | Hyaena Spotted | *Crocuta crocuta* | | |
| 31 | Hyaena Striped | *Hyaena hyaena dubbah* | | |
| 32 | Impala East African | *Aepyceros melampus rendili* | | |
| 33 | Impala Southern | *Aepyceros melampus melampus* | | |
| 34 | Jackal Common | *Canis aureus* | | |
| 35 | Jackal Side striped | *Canis adustus* | | |
| 36 | Jackal Sliver backed | *Canis mesomelas* | | |
| 37 | Klipspringer | *Oreotragus oreotragus* | | |
| 38 | Kudu Greater | *Tragelophus strepsiceros bea* | | |
| 39 | Kudu Lesser | *Tragelaphus imberbis* | | |
| 40 | Leopard | *Panthera pardus pardus* | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 41 | Lion | *Panthera leo* | | |
| 42 | Mongoose Banded | *Mungos mungo* | | |
| 43 | Mongoose White tailed | *Ichneumia albicauda* | | |
| 44 | Monkey Blue | *Cercopithecus mitis* | | |
| 45 | Monkey Velvet | *Chlorocebus pygerythrus* | | |
| 46 | Oribi Common | *Ourebia ourebi ourebi* | | |
| 47 | Oryx Fringed eared | *Oryx beisa calotis* | | |
| 48 | Ostrich | *Struthioformes camelopardalus* | | |
| 49 | Porcupine Crested | *Hystrix cristata* | | |
| 50 | Puku | *Kobus vardonii* | | |
| 51 | Python Rock | *Pythin sebae* | | |
| 52 | Ratel (Honey Badger) | *Mellivora capensis* | | |
| 53 | Reedbuck Bohor | *Redunca redunca wardi* | | |
| 54 | Reedbuck Mountain (Chandler's) | *Redunca fulvorufula chandleri* | | |
| 55 | Reedbuck Southern (Common) | *Redunca arundinum* | | |
| 56 | Roan Antelope | *Hippotragus equinus langheldi* | | |
| 57 | Sable Antelope Roosevelt | *Hippotragus niger roosevelti* | | |
| 58 | Sable Antelope Common | *Hippotragus niger kirkii* | | |
| 59 | Serval Cat | *Leptailurus serval* | | |
| 60 | Sitatunga East African | *Tragelaphus spekii spekii* | | |
| 61 | Steinbuck | *Raphicerus campestris* | | |
| 62 | Suni (Pygmy Antelope) | *Neotragus moschatus* | | |
| 63 | Topi | *Damaliscus lunatus jimela* | | |
| 64 | Warthog | *Phacochoerus africanus* | | |
| 65 | Waterbuck Common | *Kobus ellipsiprymnus ellipsiprymnus* | | |
| 66 | Waterbuck Defassa | *Kobus ellipsiprymnus defassa* | | |
| 67 | Wildcat | *Felis sylvestris lybica* | | |
| 68 | Wildebeest Eastern White bearded | *Connochaetes taurinus albojubatus* | | |
| 69 | Wildebeest | *Connochaetes taurinus* | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Western White bearded | *johnstoni* | | |
| 70 | Wildebeest Nyasa | *Connochaetes taurinus mearnsi* | | |
| 71 | Zebra Burchell's | *Equus quagga bruchelli* | | |
| 72 | Zorilla | *Ictonyx striatus* | | |
| 73 | Dove | | | |
| 74 | Duck | | | |
| 75 | Francolin | | | |
| 76 | Geese | | | |
| 77 | Guineafowl | | | |
| 78 | Pigeon | | | |
| 79 | Sandgrouse | | | |
| 80 | Spurfowl | | | |

Ninathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni sahihi kwa uelewa wangu na ninathibitisha kwamba ninaelewa matakwa ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamaporim, Sura 283 na kanuni zake.

Tarehe: ………………………….
………………………………………
Jina na
Sahihi ya Mwombaji na Mhuri wa Ofisi

KUMBUKA:

Maombi ya kibali yaambatane na nakala ya pasi ya kusafiria ya mteja na mtazamaji na nakala ya kibali cha kuingiza silaha nchini iliyoshuhudiwa na wakili.

Marekebisho ya Jedwali la Saba

19. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Saba na kuliandika upya kama ifuatavyo:

JEDWALI LA SABA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 16(8)(a))*

REJISTA YA WANYAMAPORI WALIOUAWA AU KUJERUHIWA

Jina la mteja……………………………………………………………………
Jina la Kampuni ya Uwindaji………………………………………………….
Namba ya Kibali cha Utalii wa Uwindaj……………………………...……….
Jina la Mwindaji Bing…………………………………………………………

Namba ya Leseni ya Mwindaji Bingwa……………….……..………………..

| Aina ya mnyama pori | Hali | | Silaha iliyotumika | Eneo / sehemu alipowindwa | Tarehe | Muda | Jinsia | Jira nukta ya GPS | | Urefu wa pembe, mnyama au uzito | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uawa | Jeruhiwa | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |

……………………… …………………….. …………..................
Jina jina jina

………………………. ……………………. …………………………….
Saini ya Mteja wa Uwindaji Saini ya Mwindaji Bingwa Saini ya Afisa Wanyamapori Mfawidhi

<u>UTHIBITISHO</u>

Kwa kusaini rejista hii ninathibitisha kwamba taarifa zilizojazwa ni sahihi na ukweli mtupu kwa ufahamu wangu.

……………………........ … ………………………. ………………………………....
Saini ya Mteja wa Uwindaji Saini ya Mwindaji Bingwa Saini ya Afisa Wanyama Mfawidhi

Marekebisho ya Jedwali la Kumi na Moja

20. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Kumi na Moja na kuliandika upya kama ifuatavyo:

JEDWALI LA KUMI NA MOJA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni za 20(1))*

ORODHA YA WANYAMA MUHIMU

| SN. | ENGLISH NAME | SCIENTIFIC NAME |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Buffalo (1ST, 2nd and 3rd) | *Syncerus caffer caffer* |
| 2. | Burchell's Zebra | *Equus burchellis* |
| 3. | Bushbuck | *Tragelophus scriptus* |
| 4. | Bushpig | *Potamochoerus porcus* |
| 5. | Coke' Hartebeest | *Alcelophus buselaphus cokei* |
| 6. | Common waterbuck | Kobus ellipsiprymnus |
| 7. | Eland | Taurotragus oryx |
| 8. | Defassa waterbuck | Kobus defassa |
| 9. | Gerenuk | Litocranius walleri |
| 10. | Grant's gazelle | Gazella grantii |
| 11. | Greater kudu | Tragelaphus strepsiceros |
| 12. | Hippopotamus | Hippopotamus amphibious |
| 13. | Impala | Aepyceros melampus |
| 14. | Klipspringer | Oreotragus oreotragus |
| 15. | Lesser kudu | Traelphus imberis |
| 16. | Lichteinstein's hartebeest | Alcelaphus buselaphus lichteinsteinii |
| 17. | Mountain reedbuck | Redunca furvorufula |
| 18. | Wildebeest | *Connochaetes taurinus albojubatus, Connochaetes taurinus johnstoni, Connochaetes taurinus mearnsi* |
| 19. | Oribi | Ourebia ourebi |
| 20. | Oryx | Oryx gazelle |
| 21. | Puku | Kobus vardoni |
| 22. | Roan antelope | Hippotragus equines |
| 23. | Sable antelope | Hippopotagus niger |
| 24. | Sitatunga | Tragelaphus spekei |
| 25. | Southern Reedbuck | Redunca arundinum |
| 26. | Spotted hyaena | Crocuta cricyta |
| 27. | Thomsom Gazelle | Gazella thomsonii |
| 28. | Topi | Damaliscus korrigun jimela |
| 29. | Warthog | Phacochoerus aethiopicus |

Nyongeza ya Jedwali la Kumi na Nne

21. Kanuni inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya Jedwali la Kumi na Tatu Jedwali jipya lifuatalo:

JEDWALI LA KUMI NA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 31(1))*

FOMU YA KUKATA RUFAA

1. Maelezo Binafsi ya Mrufani

(a) Jina la Mrufani: …………………………………………………………………...…
(b) Aina ya Biashara/Kazi: ……………………………………………………...……
(c) Anuani ya Posta: ……………………………………………………………...……
(d) Namba ya Simu: ……………………………………………………………………
(e) Barua-Pepe: ……………………………………………………

2. Sababu za Rufaa:

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

4. Nyaraka zilizowasilishwa kwa ajili ya Rufaa:

(a) ……………………………………………………………………………………
(b) ……………………………………………………………………………………
(c) ……………………………………………………………………………………

5. Nafuu Zinazombwa:

(a) ……………………………………………………………………………………
(b) ……………………………………………………………………………………
(c) ……………………………………………………………………………………

……………………………..  ………………..........
Sahihi ya Mrufani  Tarehe

Dodoma,
26 Machi, 2025

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*